# KASOMA HIGH SCHOOL

P.O.BOX 1382, MUSOMA
Mob: 0765 485 566, 0621 645 466, 0757 017 811.

Kumb.Na.KSS/STF/F.5/J.4/2021.

21/06/2021

MWANAFUNZI_______________________________

S.L.P. ___________

________________

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KASOMA KIDATO CHA TANO MWAKA 2021/2022.

Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule hii Julai 2021. Hongera sana.

Shule hii iko Mkoa wa Mara, Halmashauri ya wilaya ya Musoma, Tarafa ya Nyanja, Kata ya Nyamrandirira, Kijiji cha Kaboni. Umbali wa shule kutoka Makao makuu ya Mkoa ni km 50.

JINSI YA KUFIKA SHULENI

Ukifika Kituo kikuu cha mabasi cha Musoma – Bweri, utapanda daladala ya kwenda kituo cha mabasi cha zamani Musoma mjini. Hapo utapata mabasi ya kwenda Majita kupitia Majita road; Mkirira; Mugango; Nyambui; mbele kidogo teremkia kituo cha Kasoma kibaoni upande pikipiki itakayokuleta hadi shuleni. *Kwa mawasiliano zaidi* 0765 485 566 / 0621 645 466, *0757 017 811 / 0788 039 511.*

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 12/07/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 12/07/2021 kabla ya saa 12:00 jioni siku ya Jumatatu. Ofisi ya Makamu Mkuu wa shule itakuwa wazi kwa mapokezi na usajili ukiwa na:-

(i) "Pay in slip" mbili zinazoonesha malipo uliyolipia Benki.
(ii) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa kinachotolewa na Serikali.
(iii) Kivuli cha matokeo ya mtihani wa kidato cha nne (Resultslip).
(iv) Vifaa ulivyoandikiwa katika fomu hii, na fomu zilizoambatanishwa na kujazwa kwa usahihi (fomu iliyojazwa na daktari, fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi, na mzazi ya kukubali masharti ya shule).

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE YASHULE

(a) Kwa wavulana:

Ni suruali 02 za dark blue zenye marinda mawili na mifuko mitatu; miwili



Edit with WPS Office

pembeni na mmoja nyuma, zisizobana mwili ukubwa wa ”turn up” chini usipungue inchi 15 na mkanda wa ngozi rangi nyeusi.



Edit with WPS Office

(b) Kwa wasichana:

Ni sketi 02 dark blue zinazovuka magoti, zikiwa na mshono wa rinda box na mfuko mmoja



*NB: Kumbuka kushona kitambaa kizito cha suti na sio kitambaa cha sukari sukari. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka wala kuwa na ndevu shuleni.*

Kwa wasichana na wavulana:

- Shati 02 nyeupe zenye mikono mirefu, tai nyeusi, urefu usivuke mkanda wa suruali au sketi, upana sm 7 ½ na iwe na  kibanio.
- Soksi ndefu nyeupe jozi 02 zisiwe na urembo.
- Viatu vyeusi vya kamba vyenye kufunika miguu viwe na kisigino kifupi na visipige kelele wakati wa kutembea kwenye sakafu.
- Sweta dark blue aina ya “V” shingoni ya kuvaa wakati wa baridi.

(c) Rangi ya Hijab ifanane na sare ya shule. Mtandio rangi nyeupe kwa sare ya shule na rangi ya kijivu kwa sare za kazi.

(d) Sare za michezo:

- Kwa wavulana: Ni “Track suit” ya bluu, bukta na T-shirt ya rangi ya bluu yenye  shingo la mviringo (nembo itawekwa shuleni) na viatu vyeupe vya raba.
- Kwa wasichana: Ni “Track suit” ya nyekundu, bukta na T-shirt ya rangi nyekundu yenye  shingo la mviringo (nembo itawekwa shuleni) na viatu vyeupe vya raba.

(e) Sare za kazi:

- “T-shirt” 02 yenye  rangi ya damu ya mzee nzito zenye color inapatikana shuleni gharama ya Tsh.12,000/= kwa kila moja.
- Suruali 02 za rangi ya kijivu kwa wavulana na Gauni 02 mshono wa solo kitambaa cha rangi ya kijivu kwa wasichana (aje nazo).

  NB: *Mwanafunzi wa shule hii hapaswi kuja na nguo nyingine yoyote*



Edit with WPS Office

*tofauti na hizo zilizoelekezwa. Nguo za nyumbani hazitakiwi kabisa.*

ADA NA MICHANGO YA SHULE

A. Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh. 70,000/= au Tsh. 35,000/= kwa muhula. Fedha hizo zilipwe katika akaunti ya shule Na. **30301200331** Jina la Akaunti ni **KASOMA SECONDARY CAPITATION ACCOUNT**, Benki ya **NMB**. Akaunti hii ni kwa ajili ya **KARO TU**.

B. Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-
   - (i) Tsh. 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
   - (ii) Tsh. 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
   - (iii) Tsh. 20,000/= kwa ajili ya taaluma.
   - (iv) Tsh. 30,000/= kwa ajili ya kulipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
   - (v) Tsh. 2,000/= Nembo ya shule.
   - (vi) Tsh. 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza Tsh. 5,000/= na Bima ya Afya Tsh. 5,000/=.
   - (vii) Fedha ya tahadhari Tsh. 5,000/=(haitarejeshwa).
   - (viii) Mitihaninya kujipima(joint examination)Tsh. 20,000/=.

**Angalizo**: Jumla ya **Ada** na **Michango** ni **Tsh. 178,000/=**. Fedha zote za michango zilipwe Benki ya NMB kwenye Akaunti ya shule Na. **30301200332** Jina la Akaunti ni **KASOMA SECONDARY DEVELOPMENT ACCOUNT. Mwanafunzi hatapokelewa ikiwa hajamaliza michango yote shule na Ada nusu. Ada na michango iwekwe kwenye akaunti husika, usilipie kwenye akaunti moja.**

NB: HATUPOKEI PESA MKONONI, TAFADHALI LIPIA BENKI.

Vifaa vya usafi

- Fyekeo1.
- Reki 1 ya mpini wa chuma.
- Jembe 1 na mpini.
- Mifagio ya nje (Chelewa).
- Dawa ya chooni lita 5.
- Wire moja ya kuanikia nguo.
- Softbroom 01.
- Hardbroom 01.
- Squeezer rubber 01.

Vifaa vya kutumia darasani na wakati wa mitihani

- Ream 1 Double A kwa kila muhula.
- Counter Book zisizopungua 10.
- Rula ndefu1.
- Mathematical set1.
- Kalamu bluu au nyeusi zakutosha.
- Vitabu vya masomo kulingana na tahasusi yake.(Angalau kitabu kimoja kwa



Edit with WPS Office

somo).

NB: *Advanced dictionary* kwa wanafunzi wanaosoma kiingereza na *Kamusi* kwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili ni LAZIMA.

Vifaa binafsi vya kutumia bwenini

- Godoro mojala "sponge" 2 ½ x 6 .
- Chandarua.
- Galoni lita 5 kwa ajili ya kutunzia maji yakunywa.
- Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli nakikombe).
- "Toilet paper" za kutosha (Kwa matumizi yake binafsi).
- Shuka pair 02 mpya, rangi ya bluu na pinki kila pair, blanketi 1, foronya1.
- Ndala/kandambili.
- Taulo.
- Sanduku la mbao/bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake.
- Tochi/sola kwa tahadhari kama umeme ukikatika.
- Ndoo 2 ndogo za kufulia na kuogea.
- Dawa ya choo lita tano.

SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Hivyo ni muhimu kwako kumkumbusha mwanao ajue umuhimu wa nafasi hii. Ni kweli usiopingika kwamba malezi ya wanafunzi kitaaluma , kiroho na kimwili yanategemea ushirikiano kati ya walimu nawazazi.

Hivyo huna budi kumkumbusha mwanao ajue fika kwamba shuleni ni mahala pa kupata Elimu na sio mahali pa kufanya starehe na vioja. Ukosefu wa mawasiliano kati ya pande mbili katika kumuendeleza mwanafunzi kitaaluma daima huzaa wahitimu wasio na ELIMU/UJUZI. Uongozi wa shule umeona ni vizuri kuwashirikisha wazazi katika malezi ya watoto wao hasa katika kuelewa sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za jumuiya ya Shule ya Sekondari Kasoma. Hivyo hapa nakuletea sheria za shule uzisome kwa makini na kuzielewa. Aidha mwanao inambidi kuzisoma na kukiri mbele yako kuwa yupo tayari kuzitekeleza.

Mwisho, baada ya kusoma wewe mzazi/mlezi unaombwa kuweka jina na sahihi pamoja na mtoto wako aweke jina na sahihi akiahidi kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule nimuhimu.



Edit with WPS Office

(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shulehii.

(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira yashule.

(f) Kutunza mali binafsi, ya mtu mwingine na mali ya umma.

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(i) Kila mwanafunzi lazima ahudhurie "Pared Ground" kila siku asubuhi na jioni. Mwanafunzi asiyehudhuria sehemu hizo atahesabika mtoro na ataadhibiwa.

NB. *Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu awapo shuleni mzazi/mlezi anatakiwa kuwasiliana kwa kutumia namba: 0757 017811 au 0788 039511.*

<u>MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:</u>

1. Wizi.
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
6. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
7. Kufuga ndevu.
8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
9. Uvutaji wa sigara.
10. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
11. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
12. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
13. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
14. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
15. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira yashule.
16. Kudharau Bendera yaTaifa.



Edit with WPS Office

17. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
18. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

NB:
- Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki line ya simu, pasi ya umeme, redio, heater, Computer na TV akikutwa navyo atachukuliwa hatua za kinidhamu.
- Haturuhusu mwanafunzi kutembelewa na watu wasiofahamika.
- Mwanafunzi anatakiwa kuwahi sehemu yoyote anayotakiwa mara kengele inapogonga (Paredi/chakula)
- Ratiba ya shule uanza saa 11:30 alfajiri kwa kufanya usafi binafsi na mazingira ya bwenini chini ya usimamizi wa viongozi wabweni
- Mwanafunzi ataruhusiwa kusali katika dhehebu lake shuleni kwa utaratibu wa dhehebu lake kwa kuzingatia sheria zashule.

➤ <u>ADHABU:</u>
Mwanafunzi atakayekiuka utaratibu huu atasimamishwa masomo (Suspension) endapo atarudia atafukuzwa shule kabisa.



Edit with WPS Office

- **MASOMO**
    1. Mwanafunzi anatakiwa kusoma masomo yote kama alivyopangiwa na Wizara na ikiwa hatahudhuria vipindi vitano (05) mfululizo bila sababu ya msingi ataadhibiwa.
    2. Lugha rasmi ya shule ni **kiingereza** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuitumia lugha hii katika mawasiliano baina yake na walimu pia wanafunzi wenzake.

- **MIPAKA**
    1. Mwanafunzi anapofika shuleni haruhusiwi kwenda nje ya shule bila ruhusa ya MKUU WASHULE.
    2. Ni marufuku mwanafunzi kutembelea nyumba za walimu/wafanyakazi au kutoka nje ya shule bila ruhusa maalumu.
    3. Mwanafunzi atatoka nje ya shule kwa kutumia fomu maalumu iliyotolewa na MKUU WASHULE.
    4. Mwanafunzi atakayevunja sheria hii akaenda nje ya shule bila ruhusa adhabu yake ni KUFUKUZWA SHULE.

- **MAVAZI**

  Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule muda wote akiwa darasani pia haruhusiwi kujipamba na urembo wa aina yoyote.

- **CHAKULA**

  Shule haina utaratibu wa kutoa chakula maalum (Special diet) kwa wale wenye matatizo kiafya na kutokula baadhi ya vyakula.

**MAMBO MENGINE MUHIMU**

- Shule ina mihula 02 ya masomo na kila muhula unapokwisha shule hufungwa, hivyo kwa kila mzazi/mlezi anatakiwa kumtumia mwanae nauli ya kurudi nyumbani kwa ajili ya mapumziko. Shule haitaruhusu mwanafunzi kubaki shuleni wakati wa likizo ndefu.
- "Medical Examination Form" ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni pamoja na fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi na mzazi

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Tumia nafasi hii muhimu ambayo Taifa limekupa upendeleo maalumu. Ufikapo shuleni jitahidi kusoma kwa bidii ili uiokoe familia yako pamoja na Taifa kwa ujumla.

*KARIBU SANA KASOMA SEKONDARI "SHULE YENYE MAZINGIRA RAFIKI YA KUJIFUNZIA"*

MISHAEL M. ODERO
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
KASOMA SEKONDARI
S.L.P 1382
MUSOMA

Edit with WPS Office

## ORODHA YA VITABU VYA KUNUNUA

Kila mwanafunzi anatakiwa kununua anghalau kitabu kimoja kwa kila somo kwa kila tahasusi.

HISTORY

1. Essentials in Advanced level History Paper 2 Based in new (2010) Syllabus, Written by Saleh Yasin.

2. Contemporary History Events Volume l. Writen by Shibitali CK. Tumain, Shibitali and Son Publisher.

GEOGRAPHY

1. Practical Geography A-Level by Kamili. Z.

2. An Intergraded Regional Studies On Human And Economic Geography Advanced Level Paper 2 by Msabila D.T

3. A Comprehensive Approach To Physical l Geography By Msabila D.T

4. Physical Geography Alive By Kamili. Z

5. Practical Geography by Njiku. C.

ENGLISH

1. Advanced Level English: A Practical Approach (Second Edition) by Nicholous Asheli. (Paper one)

2. Advanced Level English: A Practical Approach (Second Edition) by Nicholous Asheli. (Paper two)

3. Oxford Advanced Learner's Dictionary.

KISWAHILI

1. Nadharia ya Fasihi Kidato cha 5 & 6 by J.A Masebo (2010).

2. Nadharia ya Kiswahili (kiswahili 1) Kidato cha 5 & 6 by J.A Masebo (2010).



Edit with WPS Office

3. Jikumbushe Kiswahili 2 Kidato cha 5&6 Maswali na majibu by Eliupendo W. Mbise na Leonard Mbikilwa.

4. Kamusi.

SHULE YA SEKONDARI KASOMA

FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINAKAMILILAMWANAFUNZI:______________________________________________________
2. TAREHEYAKUZALIWA:________________KABILA________________DINI________________
3. SHULE ALIYOTOKA:__________________________________________________
4. MWANAFUNZI ANATOKA MTAA WA/KIJIJI CHA__________________________
5. KATA YA:_____________________TARAFA YA_________________________
6. WILAYA YA______________________MKOA WA:_______________________
7. WAZAZI WOTE WAPO HAI/MMOJA YU-HAI/YATIMA (FUTA ISIYOHUSIKA)
8. JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI________________________________________
9. KAZI YA MZAZI/MLEZI_____________________KAMA MLEZI TAJA UHUSIANO__________
10. ANUANI YA MZAZI/MLEZI________________________SIMU____________

(a) Nimekubali nafasi niliyopewa na kuwa nitafuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Sheria zote na kanuni za shule nimezisoma na kuzielewa.

(b) Nitahakikisha na ninaahidi kuhudhuria darasani siku zote za masomo.



Edit with WPS Office

(c) Nitahakikisha nasoma kwa bidii na maarifa. Sitashiriki katika vurugu za aina yoyote ile pindi nikiwa mwanafunzi hapa Kasoma sekondari. Naahidi nitadumisha nidhamu nzuri hapa shuleni.

(d) Sitakuwa tayari kudhalilisha shule yangu.

(e) Nitakubali kuchukuliwa hatua stahiki endapo nitakapoenda kinyume na sheria za shule.

---------------------------------- ----------------------------------

JINA LA MWANAFUNZI TAREHE



Edit with WPS Office

FOMU YA AHADI YA MZAZI WA MWANAFUNZI

JINA LAMZAZI/MLEZI___________________________________________

(a) Nimesoma na kuyaelewa maelekezo na sheria za shule ya sekondari Kasoma aliyopewa mwanangu na ninakubaliana nayo.

(b) Ninakubali nafasi aliyopewa mwanangu.

(c) Nitahakikisha kuwa mwanangu anapata mahitaji yake yote muhimu ya shule.

(d) Nitakuwa bega kwa bega na walimu katika kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata sheria na kanuni zilizo shuleni. Ni dhamu nzuri ya mtoto ndiyo mafanikio yake.

(e) Naahidi kuwa mwanangu hatashiriki mgomo,fujo na wala makosa ya jinai kama yeye mwenyewe alivyoahidi. Ikitokea akikiuka hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

(f) Tafadhali jaza majina, namba za simu na kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ndugu/jamaa na mwanafunzi watakaokuja shuleni kumtembelea au kuwasiliana nae kwanjia ya simu kupitia uongozi wa shule.

| S/N | JINA | UHUSIANO | NA. SIMU | ANAKOISHI | KAZI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

-------------------------------- --------------------------------

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI TAREHE

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI …………………………………………..



Edit with WPS Office

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

KASOMA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 1382,
MUSOMA.

30/05/2020

The Medical Officer,
……………………………..
……………………………..
………………………………

RE: ………………………………………………………………………… (Full name of student).

Please kindly examine the above named as to his/her Physical and mental for enrolment as a student, the examination should include the following categories.
1. (a)Eye–Sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech (e) Venereal diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy.
2. Neurosis.
3. Pregnancy.
4. Other serious diseases.

THE HEADMASTER




PART B MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by a government Medical Officer)

I have examined the above named person and consider that he/she is physically FIT/UNFIT and mentally FIT/UNIFIT for fulltime of schooling.

1. (a)Eye–Sight……………………………………………………
(b) Hearing………………………………………………………………
(c)Limbs……………………………………………………………………(d)Speech………………………
……………………………………………………(e)Venereal diseases………………………………………………………… (f) Leprosy………………………………………………………………
(g)Epilepsy………………………………………………………………

2. Neuroses……………………………………………………………………
3. Pregnancy……………………………………………………………………
4. Other serious diseases…………………………………………………

Date ………………………………………… Signature ……………………… Station ……………………………………… Designation ………………



Edit with WPS Office

Edit with WPS Office

Edit with WPS Office

Edit with WPS Office

Edit with WPS Office